# HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA

# JARIDA LA MWEZI AGOSTI 2024

## RAIS SAMIA APONGEZA KILIMO CHA UMWAGILIAJI SINGIDA





## MKURUGENZI MPYA MANISPAA YA SINGIDA AKABIDHIWA OFISI AANZA NA MAPATO

## WAZIRI MCHENGERWA ATANGAZA TAREHE YA UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA 2024 ZA MITAA




## TUME HURU YA UCHAGUZI YAZINDUA MAANDALIZI YA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA SINGIDA



# RAIS SAMIA APONGEZA KILIMO CHA UMWAGILIAJI SINGIDA

Katika kilele cha Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Agosti 8, 2024, Viwanja vya Nzuguni, Dodoma, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa pongezi kwa jitihada za kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Singida.

Rais Samia alitoa pongezi hizi alipokuwa akitembelea vipando vya Mkoa wa Singida na kudhihirisha umuhimu wa matumizi bora ya umwagiliaji.

Rais Samia alisisitiza kwamba elimu kwa wakulima ni muhimu ili kuboresha matumizi ya umwagiliaji na kuongeza tija ya mazao.

"Uwepo wa maji ni muhimu sana kwa ustawi wa mazao yetu," alisema Rais Samia, akiweka mkazo kwenye umuhimu wa elimu ya kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima.

Pia, Rais Samia alitoa pongezi kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, kwa usimamizi mzuri wa shughuli za kilimo mkoani humo. Rais alihimiza kwamba kuendelea kutoa elimu ya kilimo cha umwagiliaji ni hatua muhimu ya kuendeleza sekta ya kilimo na kuongeza tija wa wakulima.Mkuu wa Mkoa Dendego alimhakikishia Rais Samia kuwa amepokea maagizo yake kwa umakini na kwamba mkoa wa Singida utaweka mkazo katika kutoa elimu hiyo kwa wakulima. Dendego alisisitiza kuwa mkoa utaendelea kufanya juhudi za kuhakikisha wakulima wanapata mazao ya uhakika kupitia kilimo cha umwagiliaji.

# WAZIRI MCHENGERWA ATANGAZA TAREHE YA UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA

Waziri wa nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI ) Mhe. Mohamed Mchengerwa ameutangazia Umma wa Tanzania na Vyama vya siasa kuwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tanzania Bara utafanyika tarehe 27 November 2024.

Waziri Mchengerwa ameeleza hayo leo tarehe 15 Agosti 2024 wakati akitoa Tangazo la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kuzindua nembo rasmi ya uchagunzi wenye kaulimbiu isemayo " Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi, Jitokeze kushiriki ". "Ninautangazia Umma wa Watanzania na Vyama vyote vya Siasa vyenye




Usajiri wa kudumu kuwa tarehe 27 Novemba 2024 itakuwa siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tanzania Bara, Upigaji wa kura utaanza saa mbili kamili za asubuhi na kukamilika saa kumi kamili za jioni"

Waziri Mchengerwa ameema kuwa Kampeni zitafanyika siku saba kabla ya Uchaguzi na kampeni za uchaguzi zitafanyika siku saba kabla ya uchaguzi na kubainisha kuwa kila chama cha siasa kinachoshiriki uchaguzi kitawasilisha ratiba yake ya mikutano ya kampeni ya uchaguzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi si chini ya siku saba kabla ya kuanza kampeni .

Aidha, Mchengerwa amebainisha kuwa majina na mipaka ya vitongoji yatangazwe siku 72 kabla ya uchaguzi kwa mujibu wa kanuni na kufahamisha Wananchi, majina ya maeneo na mipaka ambayo itahusika katika kujiandikisha na upigaji wa kura ambapo Wasimamizi wa Uchaguzi watatangaza majina na mipaka ya vitongoji vilivyoko katika eneo la Halmashauri husika .

Kadhalika , Waziri Mchengerwa ametoa wito kwa Wananchi kujitokeza kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kugombea na kuchagua Viongozi .

# WAZIRI PINDA ATEMBELEA BANDA LA MANISPAA YA SINGIDA

Waziri Mkuu wa Mstaafu, Mhe Mizengo Pinda, leo amefanya ziara ya kutembelea banda la Halmashauri ya Manispaa ya Singida, ambapo alikagua shughuli mbalimbali ambazo zinafanywa na wajasiriamali pamoja na kukagua mabanda ya mifugo.

Katika ziara hiyo, Pinda aliongozana na Mkuu wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe, Katibu Tawala wa Singida, Naima Chondo na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ikungi, Justin Kijazi. Hii ni katika maonesho ya Nanenane ya mwaka 2024 ambayo kitaifa yanafanyika katika Viwanja vya Nzuguni, Dodoma.

Wakati wa ziara hiyo, Pinda alitembelea mabanda ya Halmashauri zote saba, ikiwemo Manispaa, ambapo alipata nafasi ya kujionea shughuli za wajasiriamali. Aliweza kuona bidhaa mbalimbali kama vile asali, mafuta ya alizeti, unga wa lishe, na kutoa ushauri wa kuboresha ubora wa bidhaa hizo baadhi.

Aidha, Pinda alipata fursa ya kutembelea mabanda ya mifugo, ikiwa ni pamoja na ng'ombe, mbuzi, mabata, kuku, na ufugaji wa samaki, ambapo alishiriki katika majadiliano kuhusu maendeleo ya sekta hiyo. Alisisitiza umuhimu wa kuboresha bidhaa za mifugo na kuongeza ubora wa uzalishaji.



## MEYA MANISPAA AWATAKA WANANCHI KUENDELEA KUTUNZA MAZINGIRA



Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida, Mhe. Yagi Kiaratu, amesisitiza umuhimu wa kutunza mazingira kwa kuendeleza shughuli za usafi na upandaji miti.
Meya Kiaratu alitoa kauli hiyo leo mara baada ya kuhitimisha zoezi la usafi wa mazingira katika soko la Ipembe na upandaji wa miti katika barabara ya Karume.
Manispaa ya Singida, kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la Helvetas kupitia mradi wake wa SAUTI NA NAFASI, pamoja na wadau wengine, iliendesha zoezi hilo la usafi.
Katika tukio hilo, Meya Kiaratu alisema, "Leo tumefanya usafi, tumeokoa afya za wananchi. Kama tukiendelea kupanda na kutunza miti itakuwa rahisi kuwa na hali ya ukijani. Ukijani utapendezesha mji kisayansi, utaongeza usafi wa hewa, na miti itavuta mvua."
Meya Kiaratu aliongeza kuwa, "Manispaa ya Singida imekuwa mdau mkubwa katika kutunza mazingira, ndiyo maana tumekuwa tukipanda miti. Wananchi wa Manispaa tuboreshe suala la usafi; taka zisitupwe hovyo katika barabara wala mifereji. Hii itasaidia mji wetu kuwa msafi na kuvutia."

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Nchi wa Helvetas, Felix Banchman, alisema, "Zoezi hili limekuwa zuri na la pekee. Tunafurahia kuona zoezi hili linaendelea kwa pamoja, na tunatarajia kufanikisha mengi zaidi."

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Christian Kasambala, alishukuru wadau na wananchi kwa kushiriki katika zoezi hilo na kuomba kuwa jitihada hizi ziendelee ili kuimarisha mazingira na usafi wa mji.

## RC SINGIDA ATOA MAAGIZO USIMAMIZI WA MAPATO

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, amewataka viongozi wa mkoa huo kusimamia kwa karibu vyanzo vyote vya mapato na kuhakikisha kuwa taratibu zote zinafuatwa kwa usahihi.
Akizungumza katika kikao kazi kilichofanyika Agosti 29, 2024, Dendego alisisitiza umuhimu wa nidhamu ya mapato na uwajibikaji katika ukusanyaji na matumizi ya rasilimali za umma.
Mhe. Dendego alibainisha kuwa ni muhimu kwa viongozi kuhakikisha vyanzo vya mapato vinatambuliwa, kusimamiwa, na kudhibitiwa ili kuzuia mianya ya upotevu wa fedha za umma.
"Kila kiongozi anawajibika kuhakikisha mapato yanakusanywa ipasavyo na hakuna upotevu wa aina yoyote. Ni jukumu letu kuhakikisha tunasimamia rasilimali hizi kwa uadilifu na kufuata taratibu zote za kisheria," alisisitiza.
Aidha, alionya dhidi ya vitendo vya rushwa na matumizi mabaya ya ofisi, akisema kwamba viongozi wanapaswa kuwa mfano bora kwa kufuata sheria na taratibu.
"Uwazi na uwajibikaji ni msingi wa mafanikio ya mkoa. Hakuna kiongozi anayepaswa kukiuka taratibu za ukusanyaji na matumizi ya mapato," alisema Dendego.
Mkuu wa Mkoa alihimiza pia viongozi kuwa wabunifu na kutafuta vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza mapato ya mkoa na taifa kwa ujumla.
"Usimamizi mzuri wa vyanzo vya mapato utasaidia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayolenga kuboresha maisha ya wananchi wa Singida," aliongeza.
Mhe. Dendego amewataka viongozi wote kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao kwa uadilifu, wakikusanya mapato yote na kupeleka benki kwa wakati, huku wakisisitiza umuhimu wa kufuata taratibu zote zilizopo bila kuzipindisha.

## DC GONDWE AAGIZA USIMAMIZI BORA LISHE MASHULENI

Mwenyekiti wa Kamati ya Lishe Wilaya ya Singida, Mhe. Godwin Gondwe, ameendelea kusisitiza umuhimu wa usimamizi wa lishe katika kuhakikisha chakula kinapatikana katika shule za Wilaya ya Singida.

Mhe. Gondwe alitoa maelekezo haya alipokuwa akizungumza na watumishi kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Singida na

Singida DC katika kikao kilichofanyika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi.
Mhe.Gondwe alisisitiza kuwa, upatikanaji wa chakula mashuleni ni muhimu sana kwa maendeleo ya watoto kitaaluma. Aliongeza kuwa, chakula bora ni sehemu muhimu ya mazingira ya kujifunzia kwa watoto na kinachangia moja kwa moja katika utendaji wao mzuri shuleni.
"Ni lazima kuhakikisha kwamba chakula kinapatikana katika shule zote za Manispaa ya Singida. Hii siyo tu suala la lishe bali pia ni hatua muhimu katika kuboresha elimu na kuhakikisha watoto wanapata maendeleo bora," alisema Mhe. Gondwe.


Mwenyekiti huyo alibainisha kuwa usimamizi wa lishe mashuleni ni suala linalopaswa kufanyiwa kazi kwa umakini mkubwa. Aliwahimiza watumishi kuhakikisha kuwa chakula kinatolewa kwa wakati, kinakuwa na ubora, na kinakuwa sehemu ya ratiba ya kila siku mashuleni.
Aliongeza kuwa, hatua hizi zitasaidia kuondoa tatizo la watoto kukosa chakula, ambalo linaweza kuathiri uwezo wao wa kujifunza na kufanya vizuri katika masomo yao.
Aidha, Mhe. Gondwe alionya kuhusu umuhimu wa ufuatiliaji na tathmini ya hali ya lishe mashuleni. Alisisitiza kuwa, kila shule inatakiwa kuwa na mfumo mzuri wa kusimamia upatikanaji na usambazaji wa chakula, na kuhakikisha kwamba hatua zinachukuliwa pale ambapo matatizo yanajitokeza.
.



**PICHA ZA MATUKIO WAKATI WA**

**MAKABIDHIANO YA OFISI KATI YA**

**WAKURUGENZI JOANFAITH KATARAIA NA JESHI LUPEMBE TUKIO AMBALO LILI-FANYIKA AGOSTI 21, 2024.**













PICHA ZA MATUKIO WAKATI WA MAKABIDHIANO YA OFISI KATI YA

WAKURUGENZI JOANFAITH KATARAIA NA JESHI LUPEMBE TUKIO AMBALO LILIFANYIKA AGOSTI 21, 2024.





# MKURUGENZI MPYA MANISPAA AKABIDHIWA OFISI, AANZA NA MAPATO

Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Joanfaith Kataraia, amewataka watumishi wa Halmashauri hiyo kujipanga vizuri katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuitofautisha Manispaa ya Singida na Halmashauri nyingine kwa ubora, hasa katika ukusanyaji wa mapato.

Kauli hiyo aliitoa leo, Agosti 21, 2024, alipokuwa akizungumza na watumishi wa Manispaa ya Singida baada ya makabidhiano ya ofisi kati yake na mtangulizi wake, Jeshi Lupembe ambaye amehamishwa.
Kataraia amesisitiza umuhimu wa ubora na ubunifu katika utekelezaji wa shughuli, akisema kuwa Manispaa hiyo ina kila sababu ya kujitofautisha kwa namna bora.

"Tunapaswa kujiboresha katika shughuli zetu ili kuonesha utofauti kati yetu na halmashauri nyingine. Ninaimani kwa ushirikiano wetu hakuna litakaloshindikana," alisema Kataraia.

Aidha, Mkurugenzi huyo ametoa wito kwa



watumishi kutoa ushirikiano wa dhati ili kuimarisha maendeleo kupitia kuboresha utekelezaji wa majukumu katika kila idara.

Pia, amewaagiza Wakuu wa Idara na Vitengo kusimamia vizuri fedha za serikali, hasa mikopo kwa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu, na kuhakikisha zinarejeshwa kwa wakati.

"Tunapaswa kuhakikisha fedha za serikali zinarejeshwa kwa wakati na kukusanya mapato kwa usahihi ili kuepuka madeni na hoja za ukaguzi," alisisitiza.

Katika suala la utoaji huduma, Kataraia ameeleza matarajio yake ya kuona huduma bora zikitolewa kwa wananchi na kwa watumishi wenye uhitaji. Pia, amesisitiza umuhimu wa kusimamia miradi ya maendeleo kwa uangalizi mkubwa ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kwa thamani halisi ya fedha zilizotolewa. "Tusimamie miradi yote kwa nguvu zote na tutembee kwa kasi,"

**UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA , NOVEMBA 27, 2024**

## RC DENDEGO APONGEZA UJENZI WA MAJENGO YA HOSPITALI YA MANISPAA, AAGIZA UMALIZIAJI KWA KIWANGO CHA JUU

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, ameonyesha kuridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa majengo ya Mama na Mtoto pamoja na Jengo la Dharura (EMD) katika Hospitali ya Manispaa ya Singida. Mhe. Dendego alitoa pongezi na maagizo haya leo alipokuwa akifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida.
Katika ziara hiyo, Mhe. Dendego alitembelea maeneo mbalimbali ya miradi, ikiwemo Jengo la Mama na Mtoto, Jengo la Dharura, Jengo la Utawala la Manispaa, na eneo la ujenzi wa shule mpya katika Kata ya Minga. Alipokuwa katika Hospitali ya Manispaa, Mhe. Dendego alilidhishwa maendeleo ya ujenzi wa majengo hayo mawili na kusisitiza umuhimu wa umaliziaji wa miradi hiyo kwa kiwango cha juu.
"Maendeleo ya ujenzi wa majengo haya ni mazuri, lakini ni muhimu umaliziaji uwe wa kiwango cha juu," alisema Mhe. Dendego. wapongeza Mhandisi wa Manispaa, Kalisto Mligo na mafundi wake, kwa usimamizi mzuri wa mradi huo na kutaka kwamba makosa yoyote



yanayoweza kujitokeza katika umaliziaji yanarekebishwa kwa wakati. Alisisitiza kwamba hatua za mwisho za mradi lazima zikamilike kwa wakati na kwa ubora ulioanzishwa.
Mhe. Dendego alibainisha kwamba ujenzi wa majengo ya Mama na Mtoto na Dharura (EMD) utachangia pakubwa katika kuboresha huduma za afya, ambapo mama wajawazito wataweza kuhudumiwa kwa pamoja, tofauti na hali ilivyokuwa awali. Alisisitiza kuwa miradi hii ni muhimu kwa kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.
Aidha, Mhe. Dendego alitoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi zake za kuboresha miundombinu. Alisema kwamba hatua hizi zitasaidia kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora na kwamba juhudi hizi zinachangia katika maendeleo ya sekta ya afya nchini.
Katika hatua nyingine, Mhe. Dendego alisisitiza kuwa miradi yote iliyoanzishwa katika miaka mitatu iliyopita lazima ikamilike kabla ya Desemba mwaka huu. Aliweka mkazo katika umuhimu wa ufuatiliaji na usimamizi wa karibu ili kuhakikisha malengo haya yanafikiwa na miradi hiyo inakamilika kwa wakati.

UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA
JIANDIKISHE PIGA KURA
2024
OFISI YA RAIS TAMISEMI

# SINGIDA YAPOKEA TRILIONI 1.7 KUTOKA SERIKALI KUU KWA MIAKA 3

Mkoa wa Singida umepokea kiasi cha Shilingi Trilioni 1.7 kutoka Serikali Kuu katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, fedha hizi zikitumika katika miradi ya maendeleo na shughuli nyingine muhimu.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, alibainisha hayo Agosti 19, 2024, alipokuwa akihitimisha ziara ya Spika wa Baraza la Wawakilishi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Zubeir Ali Maulid. Ziara hiyo ya siku nne ilitoa fursa ya kuonyesha maendeleo yaliyopatikana mkoani Singida.
Mhe. Dendego alifafanua kuwa wastani wa mapato yaliyokusanywa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania TRA) ni Shilingi Bilioni 12.382 kwa mwaka. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, TRA imekusanya zaidi ya asilimia 101.6 ya malengo yaliyowekwa. Aidha, Halmashauri saba za Mkoa wa Singida zilikusanya mapato ya Shilingi Bilioni 16.285 kwa mwaka, ambapo kwa mwaka 2023/2024, zilikusanya mapato kwa asilimia 110, ikionesha ongezeko la mapato ya ndani.

Mhe. Dendego alieleza kuwa Shilingi Bilioni 3.068 zilitolewa kwa mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu katika miaka mitatu iliyopita. Hata hivyo, baada ya kusitishwa kwa mikopo hiyo, Shilingi Bilioni 2.258 zimetengwa kwa ajili ya vikundi hivyo baada ya mwongozo kutoka Serikali.

Kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 27, 2024, Mhe. Dendego alithibitisha kuwa Mkoa wa Singida umejiandaa kwa amani na usalama, huku akisisitiza umuhimu wa kuzingatia



misingi ya demokrasia.

Aidha, alisifu mpango wa stakabadhi ghalani ulioimarisha bei ya kilo moja ya dengu kutoka Shilingi 1,500 hadi Shilingi 2,042.

Kwa upande wake, Spika Maulid alipongeza ushirikiano mzuri uliopo kati ya Serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, akisisitiza umuhimu wa mshikamano huo kuimarishwa ili kuhakikisha uchaguzi ujao unafanyika kwa amani. Alitoa wito kwa viongozi wa Serikali na Chama kuendelea kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu ili kufanikisha malengo ya kitaifa.

## UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024

## KUFANYIKA NOVEMBA 27, 2024

# DAS SINGIDA AWAASA WATUMISHI WA AFYA

Katibu Tawala wa Wilaya ya Singida, Bi Naima Chondo, ameendelea kusisitiza watumishi wa afya katika kuboresha huduma kwa mama na mtoto ili kupunguza vifo vya mama na mtoto ndani ya Manispaa ya Singida
Kauli hiyo alitoa Agosti 20 wakati kikao cha Tathmini ya Hali ya Lishe na Jiongeze Tuwavushe Salama kwa kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka wa fedha 2023-24 kilichofanyika katika ukumbi wa Ofisi za Manispaa ya Singida,mkoani Singida.
Katika kikao hicho, taarifa ya Mama na Mtoto iliweza kujadiliwa kwa kipindi cha Aprili



hadi Juni huku lengo la Manispaa likiwa ni kutokuwa na vifo kwa mama na mtoto wakihaidi kuendelea kuboresha huduma za afya.
Bi Naima alisema watumishi wa afya wanatakiwa kuendelea kupambana na kusimamia vyema eneo hilo kuhakikisha Manispaa ya Singida inatoa huduma bora kwa mama na mtoto.
"Kama watumishi, tunapaswa kuendelea kupambana kuhakikisha tunaokoa maisha ya mama na mtoto pindi wanapojifungua,".
Hata hivyo, Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa ikipambana katika kuboresha huduma hizo hasa za mama na mtoto katika maeneo yote nchini kuanzia ngazi ya chini.

# HUDUMA BORA ZA AFYA ZASOGEZWA KARIBU YA WANANCHI WA MANISPAA YA SINGIDA

Wananchi wa Manispaa ya Singida, hususan mama wajawazito na watoto, sasa wanatarajia kupokea huduma bora za afya baada ya Serikali kuboresha miundombinu katika Hospitali ya Manispaa ya Singida.
Huduma hizo za kisasa zitaanza kutolewa hivi karibuni baada ya kukamilika kwa majengo ya Mama na Mtoto na ya Wagonjwa wa Dharura (EMD).

Daktari Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Singida, Dkt. Hamis Yuna, alieleza kwamba kukamilika kwa majengo haya mawili kutasaidia kupanua wigo wa huduma za afya na kuongeza uwezo wa hospitali kutoa huduma nyingi kwa wakati mmoja.
Dkt. Yuna alisema, "Tunaendelea na ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto pamoja na jengo la Dharura. Aidha, tunakarabati jengo la upasuaji ambalo litasaidia kuboresha huduma zetu. Hivi sasa, tunahudumia mama wajawazito 16 kwa wakati mmoja, lakini jengo jipya litakuwa na uwezo wa kuhudumia hadi mama 40 kwa wakati mmoja na kutakuwa na huduma za ziada kama chumba cha upasuaji.
Kwa upande wa jengo la dharura, eneo letu la sasa lina uwezo wa kuhudumia wagonjwa watatu pekee, lakini jengo jipya litakuwa na uwezo wa kuhudumia wagonjwa sita kwa wakati mmoja."

Dkt. Yuna aliongeza kuwa: "Kwa niaba ya wananchi wa Manispaa ya Singida, tunamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kututambua na kutuboreshea huduma za afya. Tunatarajia kwamba huduma hizi zitakuwa zimeanza rasmi ifikapo mwisho wa mwezi Septemba."
Mbali na ujenzi huo, hospitali hiyo pia inaendelea na ukarabati mkubwa wa jengo la upasuaji, ambapo huduma za upasuaji zitaanza rasmi ndani ya hospitali, hivyo kuimarisha huduma zinazotolewa kwa wananchi.

## BAADHI YA MIRADI INAYOENDELEA KUTEKELEZWA MANISPAA YA SINGIDA



***Muonekano wa Nyumba ya Mkurugenzi inaendelea na ujenzi katika hatua ya upauaji***



***Jengo la Utawala la Manispaa ya Singida ujenzi unaendelea.***

## BAADHI YA MIRADI INAYOENDELEA KUTEKELEZWA MANISPAA YA SINGIDA



***Jengo la Dharura ujenzi unaendelea ikiwa katika hatua ya ukamilishaji***



***Ujenzi wa madarasa mawili katika Sekondari ya Unyamikumbi***



***Jengo la Mama na Mtoto ujenzi ikiwa katika hatua ya ukamilishaji***

# DC SINGIDA AONGOZA KIKAO CHA ELIMU KUHUSU MFUMO WA STAKABADHI GHALA



Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhe. Godwin Gondwe, ameongoza kikao kazi kilicholenga kutoa elimu juu ya mfumo wa Stakabadhi Ghalani ulioboreshwa.Kikao hicho kilifanyika leo katika ukumbi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC) na kushirikisha Wakuu wa Idara na Vitengo, Maafisa Ugani, na Watendaji wa Kata kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Singida na Wilaya ya Singida.

Katika kikao hicho, Mhe. Gondwe alitoa maelekezo kwa maafisa ushirika kuhakikisha kuwa wakulima wanapata fedha zao kwa wakati, minada inafanyika kwa wakati, na vyama vya ushirika vinatoa huduma bora kwa wakulima. Aliagiza kuwa wakulima walipwe ndani ya saa 48, wanunuzi wasajiliwe ipasavyo, orodha za maghala na waendesha maghala ziwe wazi, na vituo vya ukusanyaji viongezwe.

Afisa Ushirika wa Mkoa wa Singida, Joseph Dachi, alieleza kwa kina kuhusu mfumo wa Stakabadhi Ghalani na jinsi ulivyoimarishwa. Mhe. Gondwe alisisitiza kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inathamini wakulima wake, na mafunzo haya ni sehemu ya juhudi za kuboresha hali ya maisha ya wakulima kwa kutoa msaada wa kitaalamu na kuhakikisha kuwa wanapata faida bora kutoka kwa mazao yao.

Mhe. Gondwe aliongeza kuwa mfumo huu utasaidia wakulima kuuza mazao yao kwa bei nzuri, tofauti na mfumo wa awali, na utakuwa rafiki kwa mkulima. Alisisitiza umuhimu wa elimu hii kwa watumishi ili waweze kutoa msaada bora kwa wakulima kuhusu mfumo huu mpya.

Afisa Ushirika, Dachi, alikiri kwamba mfumo huu utaongeza fursa kwa wakulima, utawasaidia kuuza mazao yao kwa bei nzuri, na kuboresha ufanisi katika sekta ya kilimo. Alifafanua kuwa mafunzo haya ni sehemu ya juhudi za serikali kuhakikisha wakulima wanapata huduma bora na faida kutokana na shughuli zao za kilimo, hasa kwa mazao ya dengu, mbaazi, na choroko katika Wilaya ya Singida.

# WALENGWA WASIMULIA NAMNA TASAF ILIVYOBADILISHA MAISHA WAISHUKURU SERIKALI

Walengwa wa Mradi wa TASAF wameeleza jinsi mradi wa vitofali (pavement) ulivyobadilisha maisha yao na kutoa shukrani kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa ushirikiano na msaada wao.

Akizungumza wakati wa kukabidhi mradi wa vitofali uliohitimishwa katika Shule ya Msingi Imbele, Manispaa ya Singida, walengwa walisisitiza umuhimu wa mradi huo. Mradi huo, uliofadhiliwa na TASAF, umeendeshwa na walengwa 44, ambapo mwanaume alikuwa mmoja pekee. Walengwa walihusika katika ufyatuaji wa vitofali na kutengeneza eneo la utawala la shule hiyo ili kupunguza vumbi na tope wakati wa masika.

Mradi huu umekuwa na mchango mkubwa kwa walengwa, ambao wamepata elimu ya ufundi ya ufyatuaji vitofali na wanaamini ujuzi huu utaendelea kuwa na manufaa kwao. Caroline Francis, mmoja wa walengwa, anasema: "Mradi wa TASAF umenisaidia kubadili maisha yangu. Hadi sasa nimeweza kujenga nyumba na pia nafanya biashara ndogondogo. Nashukuru Serikali yetu kwa kuendelea kutuunga mkono."

Mwinyi Masumbuko, mwanaume pekee kati ya walengwa 44, ameongeza: "Nimepita katika miradi mingi ya TASAF, lakini huu umeweza kumsaidia mtoto wangu kumaliza kidato cha nne na pia nimemudu kupata kiwanja. Ingawa fedha ni chache, tunapambana na tunashukuru Serikali."

Mratibu wa TASAF wa Manispaa ya Singida, Stara Beka, amesema: "Huu ni mradi mpya wa TASAF na umeleta mabadiliko makubwa. Walengwa wamepata ujuzi utakaowasaidia sana. Wengi tayari wapo tayari kuanzisha vikundi vitakavyokuwa msaada kwao. Tunashukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa ruzuku kwa walengwa hawa."



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Imbele, Edina Daudi, amesema: "Kama familia ya Imbele, tumenufaika sana na mradi huu. Tulikuwa tunakumbana na tatizo la vumbi na mmomonyoko wa udongo, lakini mradi huu umeleta mabadiliko makubwa. Tunamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan na timu nzima ya TASAF kwa kubadili maisha ya walengwa."

# KWAHERI MKURUGENZI JESHI LUPEMBE KARIBU MKURUGENZI JOANFAITH KATARAIA

Watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida leo, Agosti 21, 2024, walishuhudia makabidhiano rasmi ya ofisi kati ya wakurugenzi wawili baada ya mabadiliko ya vituo vya kazi yaliyopitishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe, amehamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, huku Mkurugenzi wa zamani wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Bi. Joanfaith Kataraia, akiteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida.

Akizungumza baada ya makabidhiano, Mkurugenzi anayeondoka, Jeshi Lupembe, alitoa shukrani kwa watumishi,



madiwani, viongozi wa serikali, na chama tawala kwa ushirikiano waliompatia wakati wa utumishi wake.

“Sijui nianzie wapi, lakini nataka kutoa shukrani zangu za dhati kwa ushirikiano wenu. Niwaombe muendelee kumpatia ushirikiano Mkurugenzi mpya ili ilani ya chama itekelezwe kwa asilimia 100,” alisema Lupembe.

Naye Mkurugenzi mpya, Bi. Joanfaith Kataraia, ameshukuru kwa ukaribisho na kuomba ushirikiano kutoka kwa viongozi wa serikali, chama na watumishi ili kuendeleza maendeleo ya Manispaa.

“Nimeguswa na namna ambavyo watumishi, serikali, na chama walivyokuwa wakifanya kazi na utawala wa awali. Nia yangu ni kuendeleza na kuboresha ushirikiano huu ili kusukuma mbele gurudumu la maendeleo,” alisema Kataraia.

Makabidhiano ya vituo ambayo yamefanyika leo ni sehemu ya mpango wa Rais wa kubadilishana vituo vya kazi kwa viongozi ili kuimarisha utendaji wa serikali katika maeneo mbalimbali.

# DC SINGIDA AAGIZA WATENDAJI WA KATA KUSIKILIZA KERO ZA WANANCHI KILA ALHAMISI

Katika juhudi za kuhakikisha amani na utulivu katika Manispaa ya Singida, Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhe. Godwin Gondwe, ametoa agizo kwa Watendaji wa Kata kusikiliza kero za wananchi kila Alhamisi.

Agizo hili lilitolewa leo wakati Mhe. Gondwe alipokuwa akizungumza na baadhi ya watumishi wa Manispaa ya Singida na Wilaya ya Singida katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC).

Mhe. Gondwe alisema kuwa kila Alhamisi, Watendaji wa Kata wanapaswa kutenga muda wa kupokea na kusikiliza kero za wananchi katika ofisi zao. Lengo la agizo hili ni kuhakikisha kuwa matatizo na kero zinazokabili wananchi zinatatuliwa kwa wakati, na hali ya maisha inaboreka kwa kiwango cha chini kabisa.

"Uamuzi huu ni sehemu ya juhudi zetu za kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora na wanashughulikiwa kwa umakini. Tunataka wananchi wetu waishi kwa amani na utulivu bila kero zozote. Hivyo, Watendaji wa Kata wanatakiwa kuwa na utaratibu wa kila Alhamisi wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi," alisema Mhe. Gondwe.

Agizo hili linakamilisha hatua zilizochukuliwa baada ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, kuzindua Kliniki ya Kero Mkoa wa Singida mnamo Juni mwaka huu. Kliniki hiyo imekuwa ikifanya kazi ya kusikiliza na kutatua kero mbalimbali kutoka kwa wananchi, huku ikihamasisha ufanisi katika usimamizi wa masuala ya wananchi.



Kwa sasa, Watendaji wa Kata 18 za Manispaa ya Singida wanatarajiwa kutekeleza agizo hili kwa umakini. Kila Kata itapaswa kuwa na utaratibu mzuri wa kusikiliza kero na kutoa majibu au hatua zinazohitajika katika kutatua matatizo yanayojitokeza.

Mhe. Gondwe alisisitiza kuwa, hatua hii ni muhimu katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma zinazostahili na kwamba matatizo yao yanashughulikiwa kwa haraka. Aliongeza kuwa, utaratibu huu utasaidia kuimarisha uhusiano kati ya serikali na wananchi, na kuondoa kero zinazoweza kuathiri amani na utulivu wa jamii.

# PICHA ZA MATUKIO KATIKA MAONESHO YA NANENANE







# MJUE RAYMOND MKUMBO AMBAYE NI CHACHU YA MAENDELEO KWA VIJANA MANISPAA YA SINGIDA

Kijana Raymond Mkumbo (26) amekuwa chachu ya maendeleo kwa vijana wengi wa Manispaa ya Singida kutokana na shughuli za maendeleo anazofanya kwa kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi zinazojitokeza.

Mkumbo ambaye ni zao la Mfuko wa maendeleo ya vijana, Manispaa ya Singida amesema hayo wakati wa maonesho ya nanenane kikanda yaliyofanyika jijini Dodoma ambapo amesema kujishughulisha na ujasiriamali wa mazao ya misitu hasa asali imemfanya kujulikana kupitia fursa mbalimbali za vijana.

Amesema kutokana na shughuli hiyo ameweza kujiendeleza kibiashara na kuongeza uzalishaji wa bidhaa zake kwa wingi ili kukidhi uhitaji wa wateja katika masoko mbalimbali.

Kijana huyo ameeleza kuwa amepata mafanikio mbalimbali kutokana na kujishughulisha na uzalishaji wa zao la asali na kuyataja baadhi ya mafanikio hayo kuwa ni pamoja na kuweza kuhudhuria katika makongamano mbalimbali ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi, kupata elimu ya ujasiriamali hususani katika uzalishaji wa asali kwa kutumia vifaa mbalimbali vya kisasa kama bomba la moshi,vazi la nyuki,glovuzi na vifaa vingine vinavyo tumika katika shughuli hii na kutoa ajira kwa vijana wenzake takribani vijana kumi ili waweze kushirikiana katika kuongeza uzalishaji wa hilo pamoja na bidhaa zitokana-




zo na nyuki.

Mkumbo anaiomba serikali kuweza kuwasaidia vijana wanao jishughulisha na ujasiriamali kwa kuwasaidia kuwapa mikopo ya kati na mikubwa yenye riba nafuu ambayo itawasaidia katika kukuza na kuendeleza shughuli zao za uzalishaji ili kuondokana na tatizo la ajira nchini pia kuandaa mazingira rafiki kwa vijana na wajasiriamali wadogo wadogo kuweza kujiajiri.

"…Nawashauri vijana wenzangu kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza ili muweze kujiajiri wenyewe na sio kutegemea ajiri kutoka serikalini, vijana tunaweza…."

# TUME HURU YA UCHAGUZI YAZINDUA MAANDALIZI YA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA SINGIDA

Tume Huru ya Uchaguzi (NEC) imeanza maandalizi ya zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Mkoa wa Singida.

Zoezi hilo linatarajiwa kuanza rasmi Septemba 25 hadi Oktoba Mosi mwaka huu.

Kwa kipindi chote cha siku saba, zoezi hili litafanyika katika Halmashauri saba za Mkoa wa Singida. Tume hiyo imeanzisha maandalizi ya kina, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu na mafunzo kwa wataalamu na wadau wa mkoa wa Singida. Kwa sasa, mafunzo haya yanaendelea katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

Katika hatua hii, Tume Huru ya Uchaguzi inahakikisha kwamba kila hatua inachukuliwa kwa umakini ili kurahisisha uboreshaji wa daftari la wapiga kura na kuhakikisha kuwa kila mwananchi anayejiandikisha kwa usahihi.

Halmashauri zote zinazohusika zitashirikiana na Tume katika kuhakikisha kwamba zoezi hilo linaendeshwa kwa ufanisi.

# PICHA ZA MATUKIO KATIKA MAONESHO YA NANENANE



